

SAUTI YA TSC

TOLEO NA. 66 **JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC)** AGOSTI 2026

WADAU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAKUTANA KUJADILI NA KUTAFUFA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akifungua kikao cha wadau wa Tume kilichofanyika leo katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC) jijini Dodoma kujadili suluhu za changamoto zinazowakabili walimu nchini.

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

 Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania  [tumeyautumishiwawalimutanzania](https://www.instagram.com/tumeyautumishiwawalimutanzania)

Mafanikio katika Mitihani Hujengwa kwa Maandalizi, Uadilifu na Ushirikiano

Tunapoelekea katika kipindi cha upimaji na mitihani ya kitaifa kwa wanafunzi wa Darasa la Nne, Darasa la Saba, Kidato cha Pili na Kidato cha Nne, matarajio ya wanafunzi, walimu, wazazi na jamii kwa ujumla huwa makubwa. Kwa wengi, hiki ni kipindi cha kutathmini matunda ya juhudi zilizowekwa katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa mafanikio katika mitihani hayajengwi katika siku za mwisho pekee, bali ni matokeo ya maandalizi ya muda mrefu, uadilifu na ushirikiano wa kila mdau wa elimu.

Kwa walimu, huu ni wakati wa kuendelea kusimama imara katika wajibu wao wa kuwaongoza wanafunzi kuelekea mafanikio. Zaidi ya kukamilisha silabasi, wanayo nafasi ya kufanya marejeo ya masomo, kuwasaidia wanafunzi wanaohitaji ufafanuzi zaidi na kuwajengea kujiamini wanapokaribia kufanya mitihani. Huu pia ni wakati wa kuendelea kuwahamasisha wanafunzi kuamini katika uwezo wao na kutumia maarifa waliyoyapata darasani.


Pamoja na maandalizi hayo, uadilifu unapaswa kuendelea kuwa nguzo kuu katika kipindi hiki. Walimu wanapaswa kuendelea kuwa mfano wa kuigwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na maadili ya taaluma ya

ualimu, huku wakijiepusha na vitendo vyovyote vinavyoweza kuhatarisha ufanyakaji wa mitihani kwa uaminifu. Vivyo hivyo, wanafunzi wanapaswa kutambua kuwa hakuna njia ya mkato ya mafanikio. Matokeo yenye heshima ni yale yanayotokana na juhudi, maarifa na nidhamu waliyoienga katika kipindi chote cha masomo.

Kwa upande wa wanafunzi, muda uliobaki ni wa kufanya marejeo ya masomo, kuzingatia ushauri wa walimu na kujiamini katika yale waliyojifunza. Wazazi na walezi nao wanalo jukumu muhimu la kuwapa watoto mazingira tulivu ya kujifunza, kuwahamasisha na kuwaepusha na mambo yanayoweza kuathiri utulivu wao wa kisaikolojia katika kipindi hiki muhimu.

Aidha, mafanikio ya wanafunzi katika mitihani hayawezi kupatikana kwa juhudi za mtu mmoja. Yanahitaji ushirikiano wa walimu, wanafunzi, wazazi, viongozi wa shule na wadau wengine wa elimu. Kila mmoja anapotekeleza wajibu wake kwa uaminifu na kuwajibika ipasavyo, mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji huimarika na kuongeza nafasi ya wanafunzi kufanya vizuri katika mitihani yao. Mafanikio ya mwanafunzi ni mafanikio ya jamii nzima, na msingi wake hujengwa kwa maandalizi, uadilifu na ushirikiano.

KATUNI



Mwenyekiti
Paulina M. Nkwama

Wajumbe
Revocatus P. Misonge
Mectildis F. Kapinga
Lameck S. Mbeya
Zachary A. Dida
Fatuma I. Muya
Edwin Mgenders
Asha Lubuva

Mhariri Mkuu
Artemony T. Vincent

Mhariri
Adili J. Mhina

Msanifu Kurasa
Lucas G. Ogunde

Wasiliana nasi kwa Simu: +255 756 927 131 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, **S.L.P 353, DODOMA.**





OFISI YA WAZIRI MKUU
TUME YA UTUMISHI WA WALIMU (TSC)

TUNASHIRIKI MAONESHU YA

**NANE
NANE**

AGOSTI 1- 8, 2026



KATIKA VIWANJA VYA
Nanenane - Nzuguni, **DODOMA**



88
2026

KARIBU TUKUHUDUMIE

"Tambua Soko, Zalisha kwa Tija Kutekeleza Dira 2050"



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu

WADAU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAKUTANA KUJADILI NA KUTAFUFA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, akifungua kikao cha wadau wa Tume kilichofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC) jijini Dodoma kujadili suluhu za changamoto zinazowakabili walimu nchini.

Na Mwandishi Wetu, Dodoma

Wadau wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) wamekutana jijini Dodoma kujadili changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu nchini na kuweka mikakati ya kuzitatua kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za elimu.

Akifungua kikao hicho katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete Convention Centre (JKCC), Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Mwl. Paulina Nkwama, alisema kikao hicho kinalenga kujadili masuala muhimu yanayohusu ustawi wa walimu na kuimarisha usimamizi wa huduma katika sekta ya elimu.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura ya 448, Tume ina jukumu la kusimamia masuala ya ajira, maadili na maendeleo ya walimu katika Utumishi wa Umma, hivyo utekelezaji wa majukumu hayo unahitaji ushirikiano wa karibu na taasisi mbalimbali za Serikali zinazohusika na usimamizi wa utumishi wa walimu.

Mwl. Nkwama alisema kikao hicho ni sehemu ya utaratibu wa Tume wa kukutana mara kwa mara na wadau wake ili kujadili na kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Tume.

Alieleza kuwa maazimio yatakayofikiwa yataimarisha utekelezaji wa majukumu ya Tume pamoja na taasisi washirika, na hivyo kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa walimu.

Kwa mujibu wake, kikao hicho kilijadili masuala mbalimbali ya kiutumishi, ikiwemo uhamisho wa taarifa za mishahara kwa walimu wanaohama kutoka mamlaka moja kwenda nyingine, changamoto za walimu wa masomo ya Amali, mafao yanayolipwa na Hazina, ushughulikiaji wa maombi ya kuajiriwa upya katika Utumishi wa Umma, pamoja na ongezeko la matukio ya kughushi nyaraka za uhamisho na hoja nyingine zinazohusu usimamizi wa walimu.

Alisema majadiliano hayo yamewezesha wadau kubadilishana uzoefu na kuweka mikakati ya pamoja ya kutatua changamoto zinazowakabili walimu katika maeneo mbalimbali ya kiutumishi.

"Walimu ni rasilimali muhimu katika maendeleo ya Taifa. Ufanisi wa sekta ya elimu unategemea ustawi wao, hivyo ni muhimu kuhakikisha changamoto zinazowakabili zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati ili kuongeza ari ya kazi na kuboresha ubora wa elimu inayotolewa kwa wanafunzi," alisema.

Aidha, aliwataka wadau kuendelea kuimarisha ushirikiano, uratibu na mawasiliano ili kuhakikisha changamoto zote zinazojitokeza zinashughulikiwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo.

Mwl. Nkwama pia aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuboresha ustawi wa walimu kupitia ajira mpya, upandishaji wa vyeo, kuboresha mazingira ya kazi na kuhakikisha maslahi yao yanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na taratibu.

Katika hatua nyingine, alimshukuru Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia muundo mpya wa utumishi na mishahara kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu, hatua ambayo amesema imeongeza morali na ufanisi wa utendaji kazi wa watumishi wa Tume.



Baadhi ya wadau wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa kikao hicho.

WADAU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAKUTANA KUJADILI NA KUTAFUFA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU



Watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu wakifuatilia hotuba ya ufunguzi wa kikao.

WADAU WA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU WAKUTANA KUJADILI NA KUTAFUFA UFUMBUZI WA CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WALIMU



Wajumbe wa kikao wakishiriki majadiliano kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu ajira, maadili na maendeleo ya walimu.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati), akitoa ufafanuzi kuhusu baadhi ya hoja zilizowasilishwa na wadau wakati wa kikao.



Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bi. Mectildis F. Kapinga, akitoa mchango wake wakati wa majadiliano.

NAIBU WAZIRI UMMY NDERIANANGA AIPONGEZA TSC, AHIMIZA ELIMU KWA WALIMU NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA

**Na Mwandishi Wetu,
Dar es Salaam**

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Ummy H. Nderiananga, tarehe 6 Julai, 2026 alitembelea banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Dar es Salaam.

Akiwa katika banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mhe. Nderiananga aliipongeza Tume kwa kazi nzuri inayofanya katika kusimamia na kuboresha huduma kwa walimu nchini, akieleza kuwa mchango wa Tume umeendelea kuimarisha utawala bora na utoaji wa huduma kwa walimu.

Alisema TSC inapaswa kuendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu haki, wajibu na maslahi yao ili kuwawezesha kuyafahamu na kuyalinda ipasavyo. Aidha, amewahimiza walimu kutumia fursa mbalimbali za kiuchumi, ikiwemo uwekezaji, ili kuboresha kipato na ustawi wa maisha yao.

Mhe. Nderiananga pia alitaka TSC kuimarisha ushirikiano na taasisi na vyombo vinavyosimamia utumishi wa walimu katika nchi mbalimbali ili kujifunza uzoefu na mbinu bora zitakazosaidia kuboresha zaidi utoaji wa huduma kwa walimu nchini.

Vilevile, amesisitiza umuhimu wa TSC kuendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali nchini zinazohusika na masuala ya walimu, akieleza kuwa ushirikiano huo utasaidia kuimarisha utoaji wa huduma na kuongeza ufanisi katika sekta ya elimu.

Kwa upande wa watumishi wa TSC walimueleza Naibu Waziri kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na Tume kupitia banda hilo, ikiwemo utoaji wa elimu kuhusu majukumu ya Tume, huduma zinazotolewa kwa walimu pamoja na kupokea na kutolea ufumbuzi changamoto zinazowasilishwa na wadau wanaotembelea banda hilo.



Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu), Ummy H. Nderiananga (wa kwanza kushoto), akisikiliza maelezo kutoka kwa watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) alipotembelea banda la TSC katika banda jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu kwenye Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), tarehe 6 Julai, 2026.

TSC YASHIRIKI WIKI YA UTUMISHI WA UMMA, YATOA HUDUMA KWA WANANCHI DODOMA



Naibu Waziri Ummy H. Nderiananga (wafuata kushoto), akiwafanyia kipeperushi kinaeleza majukumu na huduma mbalimbali zinazotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) alipotembelea banda la TSC katika Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (Sabasaba), tarehe 6 Julai, 2026.



Naibu Waziri Ummy H. Nderiananga (katikati), akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) alipotembelea banda la Tume, ambapo ameipongeza TSC kwa kazi nzuri ya kuhudumia walimu na kuisitiza kuendelea kutoa elimu kwa walimu pamoja na kuimarisha ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi ili kuboresha utoaji wa huduma, tarehe 6 Julai, 2026.

KATIBU WA TSC ATEMBELEA BANDA JUMUISHI LA OFISI YA WAZIRI MKUU SABASABA

**Na Mwandishi Wetu –
Dar es Salaam**

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama, tarehe 5 Julai, 2026 alitembelea Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam.

Katika ziara hiyo, Mwl. Nkwama alitembelea mabanda ya taasisi mbalimbali zilizochini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na kupata maelezo kuhusu majukumu, huduma pamoja na mafanikio yanayopakikana kupitia utekelezaji wa shughuli za taasisi hizo.

Akiwa katika banda hilo, alisikiliza maelezo yaliyotolewa na watoa huduma kutoka taasisi mbalimbali, waliomueleza namna Serikali inavyoendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi kupitia programu na mifumo mbalimbali ya kisasa.

Mwl. Nkwama alieleza kufurahishwa na namna taasisi zilizochini ya Ofisi ya Waziri Mkuu zinavyoshirikiana katika kutoa huduma na elimu kwa wananchi, akibainisha kuwa ushirikiano huo unaongeza ufanisi wa Serikali katika kuwahudumia Watanzania.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ni miongoni mwa taasisi zinazoshiriki katika Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo inaendelea kutoa elimu na huduma mbalimbali zinazohusu usimamizi wa utumishi wa walimu kwa wananchi wanaotembelea maonesho hayo.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati), katika picha ya pamoja na watoa huduma wa taasisi mbalimbali zilizopo ndani ya Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu mara baada ya kutembelea banda hilo katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina Nkwama (katikati), akisikiliza maelezo kutoka kwa mmoja wa watoa huduma alipotembelea Banda Jumuishi la Ofisi ya Waziri Mkuu katika Maonesho ya 50 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (Sabasaba), yanayoendelea katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere jijini Dar es Salaam.



MIAKA 10 YA TSC YAIMARISHA USHIRIKIANO NA WADAU KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Korogwe

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Korogwe imefanikiwa kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali wa sekta ya elimu katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake mwaka 2016, hatua iliyochangia kuboresha utoaji wa huduma za kiutumishi kwa walimu.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Korogwe, Bi. Angelina Msabaha, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano wa TSC Makao Makuu kuhusu mafanikio ya Tume katika kipindi cha miaka 10 ya utekelezaji wa majukumu yake.

Bi. Msabaha alisema kuwa TSC imeendelea kushirikiana kwa karibu na Idara za Elimu katika Halmashauri

ya Mji wa Korogwe na Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe pamoja na Chama cha Walimu Tanzania (CWT), ushirikiano ambao umeongeza ufanisi katika kushughulikia masuala ya kiutumishi ya walimu.

Alisema kuanzishwa kwa TSC kumeondoa ulazima wa walimu kusafiri kwenda Makao Makuu au ngazi ya mkoa kufuata huduma za kiutumishi, kwani huduma za ajira, madaraja, maadili na nidhamu sasa zinapatikana katika ngazi ya wilaya.

Kwa mujibu wake, hatua hiyo imechangia kupunguza muda ambao walimu walikuwa wakisubiri kupandishwa madaraja au kubadilishiwa miundo ya utumishi baada ya kujiendeleza kitaaluma.

Aidha, alisema matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Walimu (TSCMIS) yameongeza ufanisi katika usimamizi wa taarifa za walimu,

usajili, utoaji wa barua za ajira na mikataba pamoja na utatuzi wa changamoto mbalimbali kwa uwazi na kwa wakati.

“Kuanzishwa kwa mfumo wa TSCMIS kumepunguza gharama za walimu kusafiri mara kwa mara kufuata huduma, kuokoa muda na kuwawezesha kutumia muda mwingi zaidi kufundisha wanafunzi,” alisema Bi. Msabaha.

Pia aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za walimu, ikiwemo kupandisha madaraja, kubadilisha miundo ya utumishi kwa waliojiendeleza kitaaluma, kulipa malimbikizo ya mishahara, madai ya nauli za likizo na posho za uhamisho.

Alisema kuwa kati ya mwaka 2021



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Korogwe, Bi. Angelina Msabaha, akitekeleza majukumu yake ofisini.

MIAKA 10 YA TSC YAIMARISHA USHIRIKIANO NA WADAU KATIKA KUWAHUDUMIA WALIMU

na 2026, TSC Wilaya ya Korogwe imefanikiwa kuwapandisha madaraja walimu 3,910, ambapo walimu 2,065 ni wa shule za msingi na 1,845 ni wa shule za sekondari.

Bi. Msabaha alieleza pia kuwa utekelezaji wa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara umechangia kuwajengea walimu wapya uelewa kuhusu maadili ya kazi, muundo wa utumishi wa umma na namna bora ya kutekeleza majukumu yao katika jamii.

Alisema mafunzo hayo yamesaidia kupunguza makosa ya kinidhamu kwa kuwa walimu hupata elimu kuhusu wajibu wao kabla ya kuripoti katika vituo vya kazi.

Kwa upande mwingine, alisema TSC imeendelea kufuatilia na kusimamia ulipaji wa madaai ya

mishahara (arrear) na stahiki mbalimbali za walimu zilizohakikiwa, ambapo Serikali imekuwa ikizilipa moja kwa moja kwenye akaunti za walimu husika.

Aidha, Tume imeandaa na kusambaza miongozo mbalimbali katika shule zote za Wilaya ya Korogwe ili kuongeza uelewa wa walimu kuhusu haki zao, wajibu wao na taratibu za kushughulikia changamoto wanazokutana nazo katika utumishi.

Kwa mujibu wa Bi. Msabaha, elimu hiyo imechangia kupunguza vitendo vya utoro, ukiukwaji wa maadili ya taaluma ya ualimu na makosa mengine ya kinidhamu yanayoweza kuhatarisha ajira za walimu.

Aliongeza kuwa TSC imeendelea kufanya ziara za mara kwa mara shuleni kutoa elimu kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma za

mwaka 2022 pamoja na Kanuni za Utumishi wa Walimu za mwaka 2016.

Alisema elimu hiyo hutolewa kupitia mafunzo katika vituo vya kazi, semina elekezi, vikao kazi, ushauri na unasihi kwa kushirikiana na wakuu wa shule, pamoja na kuwajengea uwezo wa kutambua viashiria vya changamoto za kitabia kama vile msongo wa mawazo na matumizi mabaya ya pombe ili kuwasaidia walimu kabla ya kuingia katika makosa ya kinidhamu.

Vilevile, TSC imeendelea kutumia makundi ya kitaaluma katika mitandao ya kijamii na kusambaza vipeperushi vya Ijue Tume ya Utumishi wa Walimu Ngazi ya Wilaya ili kuhakikisha taarifa muhimu zinawafikia walimu kwa wakati na kuongeza uelewa kuhusu huduma zinazotolewa na Tume.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Korogwe, Bi. Angelina Msabaha (wa pili kutoka kulia), akizwa na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Korogwe.

SERIKALI YAAJIRI WALIMU 14,074 KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/26

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Serikali imeajiri jumla ya walimu 14,074 katika mwaka wa fedha 2025/26, wakiwemo walimu 4,633 wa shule za msingi na walimu 9,441 wa shule za sekondari, ikiwa ni sehemu ya jitihada za kuimarisha utoaji wa elimu nchini.

Taarifa hiyo ilitolewa hivi karibuni na Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Fatuma Muya, alipowasilisha

taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026 katika kikao cha Kamati ya Ukaguzi ya Tume.

Bi. Muya alisema katika kipindi hicho walimu 10,532 walisajiliwa, wakiwemo walimu 2,646 wa shule za msingi na walimu 7,886 wa shule za sekondari, huku taratibu za kukamilisha usajili wa walimu wengine 6,188 zikiendelea.

Aliongeza kuwa walimu 4,134 waliwasilisha maombi ya kubadilishiwa vyeo baada ya

kujiendeleza kielimu, ambapo walimu 3,251 ni wa shule za msingi na walimu 883 ni wa shule za sekondari.

Aidha, alisema walimu 15,634 walithibitishwa kazini katika kipindi hicho, wakiwemo walimu 5,803 wa shule za msingi na walimu 9,831 wa shule za sekondari.

Akizungumzia maendeleo ya upandishaji wa vyeo, Bi. Muya alisema walimu 73,380 walikasimiwa kupandishwa vyeo katika mwaka wa fedha 2025/26, ambapo walimu 48,927 ni wa shule za msingi na walimu 24,453 ni wa shule za sekondari.

Alisema kati ya hao, walimu 52,056 tayari wamepandishwa vyeo, wakiwemo walimu 34,675 wa shule za msingi na walimu 17,381 wa shule za sekondari, huku zoezi la uidhinishaji wa mishahara kwa watumishi waliopandishwa vyeo likiendelea.

Katika hatua nyingine, Bi. Muya alisema Tume ya Utumishi wa Walimu imeratibu mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wanaoshughulikia mafao ya walimu yanayolipwa na Hazina, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma hiyo.

Alisema kwa sasa Tume ya Utumishi wa Walimu inasimamia walimu 312,897 nchini, ambapo walimu 196,012 ni wa shule za msingi na walimu 116,885 ni wa shule za sekondari.



Mkurugenzi wa Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Bi. Fatuma Muya, akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Sehemu ya Ajira na Maendeleo ya Walimu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Juni 2026 katika kikao cha Kamati ya Ukaguzi cha Tume kilichofanyika hivi karibuni.

TSC YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WANANCHI KATIKA MAONESHU YA NANENANE 2026

Na Mwandishi Wetu – Dodoma

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina M. Nkwama, ametoa elimu kwa wananchi waliotembelea banda la Tume katika Maonesho ya Nanenane mwaka 2026 yanayoendelea katika Viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma, yakiwa na kaulimbiu isemayo "Tambua Soko, Ongeza Tija, Tekeleza Dira 2050."

Akizungumza na wananchi waliotembelea banda hilo, Mwl. Nkwama alisema mwalimu ana wajibu mkubwa wa kumlea mwanafunzi kwa ukamilifu, ikiwa ni pamoja na kumkuza kitaaluma, kimwili, kiroho, kijamii na kisaikolojia ili awe raia mwenye maarifa, maadili na uwezo wa kuchangia maendeleo ya Taifa.

Alieleza kuwa pamoja na jukumu la kufundisha, mwalimu anapaswa kutekeleza majukumu yake kwa uadilifu, weledi na kuzingatia maadili ya taaluma ya ualimu, kwa kuwa yeye ni mlezi na mfano wa kuigwa katika kuwajenga watoto na vijana wenye maadili mema na uzalendo.

Mwl. Nkwama alisisitiza pia umuhimu wa ushirikiano kati ya walimu, wazazi na walezi

katika kuhakikisha maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma, kitabia na kijamii, akieleza kuwa mafanikio ya mwanafunzi yanahitaji mchango wa kila mdau.

Aidha, aliwahasisha watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla kuendelea kuthamini mchango wa walimu kwa kutembelea na kuwajulia hali walimu waliowafundisha, hususan wa elimu ya awali na msingi, ambao waliweka msingi wa mafanikio yao ya kielimu na maisha kwa ujumla.

Alisema kuwa ushiriki wa TSC katika Maonesho ya Nanenane unalenga kutoa elimu kuhusu majukumu na huduma zinazotolewa na Tume, sambamba na kuhamasisha jamii kutambua nafasi muhimu ya mwalimu katika kujenga rasilimali watu yenye maarifa, maadili na ujuzi. Alibainisha kuwa elimu bora ndiyo msingi wa kuongeza tija katika sekta zote za uzalishaji na kufanikisha utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.



Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwl. Paulina M. Nkwama, akitoa elimu kwa wananchi waliotembelea banda la Tume katika Maonesho ya Nanenane mwaka 2026 yanayofanyika katika Viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.

TSC YAENDELEA KUTOA ELIMU KWA WANANCHI KATIKA MAONESHU YA NANENANE 2026



Huduma zikiendela kutolewa katika banda la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwenye maonesho ya Nanenane yanayoendelea katika Viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma.

WALIMU WA WILAYA YA KOROGWE WAPONGEZA JITIHADAZA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

Na Mwandishi Wetu – Korogwe

Baadhi ya walimu wa Wilaya ya Korogwe wamepongeza jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu kwa muda mrefu na kuboresha mazingira ya kazi.

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Korogwe inahudumia jumla ya walimu 2,553, ambapo walimu 1,526 ni wa shule za msingi na walimu 1,027 ni wa shule za sekondari.

Wakizungumza hivi karibuni kuhusu mafanikio yaliyopatikana chini ya Serikali ya Awamu ya Sita, walimu hao walisema hatua zilizochukuliwa zimeongeza ari ya kazi na kuboresha utoaji wa huduma za elimu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Buna, Bw. Adriano Godfrey Mhina, alisema Serikali imeendelea kutekeleza upandishaji wa madaraja kwa walimu, jambo ambalo limeongeza motisha na kuimarisha hali ya kujiamini miongoni mwao.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Mbeza Mazoezi, Bi. Zvena Twaha Hassan, akitekeleza majukumu yake ya kufundisha wanafunzi.

Alisema pia Serikali imeboresha maslahi ya walimu, mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuongeza walimu wa masomo ya sayansi na biashara, hali iliyochangia kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi kutokana na uwepo wa mazingira bora ya utoaji wa elimu.

Aidha, Bw. Mhina aliiomba Tume ya Utumishi wa Walimu kuendelea kushirikiana kwa karibu na walimu ili

kutatua changamoto zinazowakabili na hivyo kuongeza ufaulu wa wanafunzi katika ngazi ya shule, wilaya, mkoa na taifa.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mbeza Mazoezi, Bi. Zvena Twaha Hassan, alisema juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita zimeboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji kupitia ongezeko la vifaa vya kufundishia pamoja na kuboresha maslahi ya walimu.

Aliiomba Serikali kuendelea kuboresha mishahara na stahiki za walimu, kuimarisha miundombinu ya shule ikiwemo madarasa, vyoo na nyumba za walimu, pamoja na kuhakikisha vifaa vya kufundishia na kujifunzia vinapatikana kwa wingi.

Bi. Zvena alisema hatua hizo zitachangia kuongeza ufaulu wa wanafunzi, kuimarisha nidhamu shuleni, kuongeza mahudhurio ya wanafunzi na kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji.

Aidha, alipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, akisema imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa ufanisi katika kusimamia maadili, nidhamu, ajira na maendeleo ya walimu.



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Buna, Bw. Adriano Godfrey Mhina, akitekeleza majukumu yake ya ufundishaji darasani.

WALIMU WASHAURIWA KUSOMA NYARAKA ZINAZOPATIKANA KWENYE TOVUTI YA TSC

Na Mwandishi Wetu – Muheza

Walimu wa shule za umma nchini wameshauriwa kusoma nyaraka mbalimbali zinazopatikana kwenye tovuti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ili kuongeza uelewa wao kuhusu sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia utumishi wa walimu.

Wito huo umetolewa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Muheza, Bw. Pachal Qamara, wakati wa mahojiano na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

Bw. Qamara alisema kuwa nyaraka zinazopatikana kwenye tovuti ya Tume, ikiwemo Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Na. 25 ya mwaka 2015, Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma Tanzania Bara, Mwongozo wa Usimamizi wa Maadili na Nidhamu Ngazi ya Shule pamoja na Mwongozo wa Masuala ya Ajira na Maendeleo ya Walimu, zimeandaliwa ili kuwasaidia walimu kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizopo.

Alieleza kuwa Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya pamoja na vitabu vinavyofafanua kanuni za maadili na utendaji kazi katika utumishi wa walimu vimekuwa na mchango mkubwa katika kuwawezesha walimu wapya kuanza kazi kwa ufanisi na kupunguza makosa ya kiutumishi.

“Ofisi ya Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Muheza inaendelea kuwashauriwa na kuwahamasisha walimu pamoja na wadau wengine kutumia tovuti ya Tume ili kupata taarifa mbalimbali muhimu, sheria, kanuni na miongozo itakayowaongezea uelewa kuhusu utumishi wa walimu,” alisema Bw. Qamara.

Akizungumzia mafanikio yaliyopatikana, Bw. Qamara alisema kuwa walimu 501 wa ajira mpya wamesajiliwa katika Wilaya ya Muheza tangu kuanzishwa kwa Tume, hatua ambayo imechangia kuimarisha utoaji wa huduma za elimu kwa wananchi.


Aliongeza kuwa Tume kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza imefanikiwa kutoa mafunzo elekezi kwa walimu 96 wa ajira mpya katika miaka ya fedha 2024/2025 na 2025/2026, ambapo walimu 24 ni wa shule za msingi na 72 ni wa shule za sekondari.

Kwa upande wa maendeleo ya walimu, alisema kuwa katika mwaka wa fedha 2025/2026, walimu 286 walistahili kupandishwa madaraja, huku walimu 256 wakiwa tayari wamekasimiwa madaraja hayo kufikia mwisho wa Juni, 2026.

Aidha, alisema walimu 24 walijajiriwa katika Wilaya ya Muheza kati ya mwezi Februari na Juni katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Bw. Qamara aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuwekeza katika kuboresha miundombinu ya elimu, ikiwemo ujenzi wa shule mpya za sekondari za Manofu na Kwabastola, shule za msingi za Jambe na Kwemsala, pamoja na ujenzi wa maabara katika shule za sekondari za Kwabastola, Chief Mang’anya, Mkurumuzi na Muhamba.

Aliongeza kuwa Serikali pia imejenga vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali za msingi zikiwemo



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Muheza, Bw. Pachal Qamara, akizungumza na Maafisa wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini wakati wa mahojiano kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika kuwahudumia walimu chini ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Misufini, Jibandeni, Magoda, Mgoda na Mwembeni, pamoja na shule za sekondari za Chartur, Kwabastola, Chief Mang’anya, Muhamba, Misozwe, Muheza High School, Pande Darajani, Edward Fumbwe na Kwabada, hatua iliyoboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia.

Kwa mujibu wa Bw. Qamara, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutatua changamoto mbalimbali za walimu ikiwemo kupandishwa madaraja, kubadilishiwa miundo ya kada, kulipwa malimbikizo ya mishahara pamoja na madai ya nauli.

Alisema kuwa kati ya mwaka 2021 hadi 2026, jumla ya walimu 2,307 wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Muheza wamepandishwa madaraja.

Wakati huo huo, baadhi ya walimu wa Wilaya ya Muheza wameipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa juhudi zake za kuboresha mazingira ya kazi na kuinua sekta ya elimu.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Chief Mang’anya, Mwl. Fikirini Twaha Mtana, alisema Serikali imeendelea kuboresha maslahi ya walimu pamoja na mazingira ya kujifunzia na kufundishia kupitia ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Aliongeza kuwa utoaji wa posho ya kufundishia (Teaching Allowance) pamoja na kupandishwa madaraja kwa walimu umeongeza motisha ya kazi na kuchangia kuimarika kwa ufaulu wa wanafunzi.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Msingi Majengo, Mwl. Josina Victory Ungele, aliomba Serikali kuendelea kutoa mafunzo kuhusu mtaala mpya kwa walimu mara kwa mara na kuongeza ajira za walimu wa shule za msingi ili kupunguza uwiano mkubwa wa wanafunzi kwa mwalimu darasani.

Aidha, aliishukuru Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuendelea kushughulikia changamoto mbalimbali za walimu kwa wakati.

TSC PANGANI YAISHUKURU SERIKALI KWA KUGHARAMIA UCHAPISHAJI WA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA

Na Mwandishi Wetu, Pangani

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Pangani imeishukuru Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuiwezesha Tume kuchapisha Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya wanaoajiriwa katika Utumishi wa Umma.

Hayo yamesemwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Pangani, Mwl. Kaunga J. Kaunga, alipokuwa akielezea mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya elimu chini ya Serikali ya Awamu ya Sita.

Mwl. Kaunga alisema kuwa Mwongozo huo umekuwa nyenzo muhimu ya kuwajengea uwezo walimu wapya kwa kuwafahamisha sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, jambo ambalo limechangia kupunguza changamoto za kinidhamu miongoni mwa walimu wanaoajiriwa.

Alieleza kuwa pamoja na kuwasaidia walimu kuelewa wajibu na haki zao, mwongozo huo pia



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Pangani Halisi, Wilaya ya Pangani, Mwl. Anjelina Ludovick Clemensi, akiendesha kipindi darasani.

unawakumbusha waajiri kutekeleza kwa wakati wajibu wao wa kulipa stahiki mbalimbali za walimu wa ajira mpya, huku ukiboresha mawasiliano na ushirikiano kati ya walimu na waajiri.

Aidha, alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa walimu kupitia utatuzi wa changamoto mbalimbali, ikiwemo upandishaji wa madaraja na marekebisho ya miundo ya utumishi, hatua ambazo zimeongeza ari na motisha wa walimu katika kutekeleza majukumu yao.

Alisema katika mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Pangani ilifanikiwa kupandisha vyeo walimu 65, wakiwemo 46 wa shule za msingi na 19 wa shule za sekondari.

Mwl. Kaunga pia aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu ya elimu wilayani humo, ambapo imejenga madarasa mapya katika Shule za Msingi Boza, Mwera, Kipumbwi, Kipumbwi Pwani, Mkalamo, Mkwaja, Masaika na Kigusimba, pamoja na

kufanya ukarabati wa shule kongwe za msingi.

Aliongeza kuwa Serikali imejenga shule mpya nne za sekondari ambazo ni Shule ya Sekondari Jumaa Aweso, Shule ya Sekondari Masaika, Shule ya Sekondari Muhembo na Shule ya Sekondari Pangani Halisi, zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja.

Akizungumzia maendeleo ya walimu, Mwl. Kaunga alisema kuwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2026, Serikali ya Awamu ya Sita imepandisha madaraja walimu 598 wilayani Pangani, ambapo 335 ni walimu wa shule za msingi na 263 ni walimu wa shule za sekondari.

Katika hatua nyingine, alisema Ofisi ya Tume imeendelea kutoa elimu kwa walimu kupitia ziara katika shule 42, ambapo imekuwa ikiendesha mikutano ya uelimishaji na kusambaza nakala za kidijitali za Kanuni za Tume ya Utumishi wa Walimu za Mwaka 2016 pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2022, kwa lengo la kuongeza uelewa kuhusu haki, wajibu na maadili ya utumishi.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Pangani, Mwl. Kaunga J. Kaunga, akiendelea kutekeleza majukumu yake ofisini hivi karibuni.

TSC PANGANI YAISHUKURU SERIKALI KWA KUGHARIMIA UCHAPISHAJI WA MWONGOZO WA MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WAPYA



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Pangani Halisi, Wilaya ya Pangani, wakiwa katika picha ya pamoja na mwalimu wao baada ya kipindi cha masomo.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Kimang'a, Wilaya ya Pangani, Mwl. Fatuma Mbwana Mwinjuma, akifundisha wanafunzi darasani.

MAFUNZO ELEKEZI KWA WALIMU WA AJIRA MPYA YAIMARISHA UTENDAJI KAZI WILAYANI MKINGA

Na Mwandishi Wetu, Mkinga

Mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya yanayotolewa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkinga yamechangia kuimarisha uelewa wa walimu kuhusu sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma, hatua iliyosaidia kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa TSC Wilaya ya Mkinga, Bw. Juma M. Seleman, wakati akizungumza kuhusu mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa huduma kwa walimu wilayani humo.

Bw. Seleman alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo walimu wa ajira mpya kuhusu maadili na nidhamu ya utumishi wa umma, jambo lililochangia kupunguza kwa kiwango kikubwa ukiukwaji wa maadili na mashauri ya kinidhamu.

Alisema idadi ya mashauri ya kinidhamu imepungua kutoka mashauri matatu (3) mwaka 2023 hadi kutokuwepo kabisa kwa shauri lolote (0) mwaka 2026.

Alifafanua kuwa matumizi ya Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya Wanaojiriwa katika Utumishi wa Umma yamewawezesha walimu kuelewa wajibu na haki zao, hivyo kupunguza migogoro kati yao



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Mkinga, Bw. Juma M. Seleman, akitoa mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya.

na mwajiri.

Akizungumzia matumizi ya teknolojia, Bw. Seleman alisema kuanzishwa kwa Mfumo wa TSCMIS kumeborisha utoaji wa huduma kwa walimu kwa kurahisisha usajili wa walimu, utoaji wa barua za ajira,

uthibitisho kazini pamoja na usimamizi wa mikataba ya ajira kwa wakati.

Aidha, alisema mfumo huo umeongeza ufanisi katika usimamizi wa mashauri ya kinidhamu kwa kuwezesha taarifa kupatikana na kushughulikiwa kwa haraka, tofauti na ilivyokuwa awali ambapo maamuzi yalichukua muda mrefu kutolewa.

Katika hatua nyingine, Bw. Seleman alisema Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuboresha maslahi ya walimu kwa kuharakisha upandishaji wa vyeo, mabadiliko ya miundo kwa walimu waliojiendeleza kielimu pamoja na ulipaji wa stahiki mbalimbali kwa wakati.

Aidha, alisema TSC Wilaya ya Mkinga imeendelea kutoa elimu kwa walimu kupitia mikutano inayoratibiwa na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, mafunzo elekezi, ziara za kutembelea shule pamoja na kuhakikisha kila shule inakuwa na nakala ya mwongozo wa maadili na taratibu za utumishi. Hatua hizo zimechangia kuwajengea walimu uelewa na kuwakinga dhidi ya ukiukwaji wa maadili ya kazi.

Kwa upande wa maendeleo ya taaluma, Bw. Seleman alisema kuanzia mwaka 2024 hadi 2026 jumla ya walimu 760 wamebadilishiwa miundo baada ya kujiendeleza kielimu.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Bw. Michael Mbilu (kulia), akiwa pamoja na maafisa wengine wakati wa mafunzo elekezi kwa walimu wa ajira mpya wilayani Mkinga.

WAALIMU WILAYANI KIBAHA WAIPONGEZA TSC KWA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA



Mwalimu Solomon C. Mkindege wa Shule ya Sekondari Miembe Saba, Manispaa ya Kibaha, akieleza mafanikio ya TSC katika kuboresha huduma za kiutumishi kwa walimu.

Na Mwandishi Wetu, Kibaha

Walimu wa Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, wameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kwa kuendelea kuboresha utoaji wa huduma za kiutumishi na kushughulikia kwa wakati changamoto mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili walimu kwa muda mrefu.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti kuhusu mafanikio ya TSC katika kipindi cha miaka 10 tangu kuanzishwa kwake, walimu hao walisema Tume imeleta maboresho makubwa katika usimamizi wa masuala ya kiutumishi, ikiwemo upandishaji wa madaraja, ulipaji wa stahiki, usimamizi wa mashauri ya kinidhamu, pamoja na kusogeza huduma karibu na walimu kupitia ofisi za wilaya.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Miembe Saba, Halmashauri ya Manispaa ya Kibaha, Solomon C. Mkindege, alisema moja ya mafanikio makubwa ya TSC ni kuondoa changamoto zilizokuwa zikijitokeza katika upandishaji wa madaraja na ulipaji wa stahiki za walimu.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa TSC, walimu wengi walikuwa wakikabiliwa na ucheleweshaji

wa kupandishwa madaraja na kulipwa stahiki zao, hali iliyokuwa ikisababisha malalamiko ya muda mrefu. Hata hivyo, kwa sasa walimu wengi hupandishwa madaraja na kulipwa stahiki zao kwa wakati, jambo ambalo limeongeza ari, motisha na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

Aidha, alisema TSC imefanikiwa kutatua changamoto iliyokuwa

ikiwakabili walimu wanaojiendeleza kielimu kuhusu mabadiliko ya muundo wa kada. Alieleza kuwa hapo awali walimu waliobadilishiwa muundo walikumbana na athari katika tarehe zao za kupandishwa madaraja, lakini kwa sasa utaratibu huo umeboreshwa na haki zao za kupanda madaraja zinalindwa.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Msingi Mwendopole, Kemilembe Mhunge Kasilima, alisema katika kipindi cha miaka 10 ya TSC, miongozo mbalimbali ya kiutumishi imetolewa na kuwasaidia walimu kuelewa kwa kina haki, wajibu na taratibu za utumishi wa umma.

Alisema kupitia miongozo hiyo, walimu wameongeza uelewa kuhusu masuala yanayohusu maslahi yao, yakiwemo fedha za kujikimu, likizo, uhamisho pamoja na maadili ya utumishi wa umma.

Mwalimu Kemilembe pia alipongeza TSC kwa kusogeza huduma karibu na walimu kupitia uanzishwaji wa ofisi katika ngazi ya wilaya.

“Kwa sasa tunapata huduma karibu nasi. Maafisa wa TSC wanapatikana kwa urahisi na changamoto zetu zinapatiwa ufumbuzi kwa wakati. Hali hii ni tofauti na ilivyokuwa awali ambapo



Mwalimu Kemilembe Mhunge Kasilima wa Shule ya Msingi Mwendopole akizungumza kuhusu mchango wa TSC katika kusogeza huduma karibu na walimu na kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

WAALIMU WILAYANI KIBAHA WAIPONGEZA TSC KWA KUIMARISHA UTOAJI WA HUDUMA



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Kibaha, Bw. Marco Bahebe, akizungumza wakati wa mahojiano na Afisa wa Mawasiliano Serikalini kutoka TSC Makao Makuu ofisini kwake wilayani Kibaha.

walimu walilazimika kufuata huduma katika ofisi za mkoa,” alisema.

Naye Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu Wilaya ya Kibaha, Bw. Marco Bahebe, alisema uwepo wa ofisi za TSC katika kila wilaya ni miongoni mwa mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 10 ya Tume.

Alisema hatua hiyo imeongeza upatikanaji wa huduma kwa walimu, kurahisisha utatuzi wa changamoto zao pamoja na kupunguza muda na gharama walizokuwa wakitumia kufuata huduma katika ngazi ya mkoa.

Aidha, alisema TSC imeendelea kuandaa rejea na miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa majukumu yake, ikiwemo miongozo iliyochapishwa kwa maandishi ya Braille kwa walimu wenye uoni hafifu na wasioona.

Alisema hatua hiyo imeongeza ushirikishwaji na usawa kwa kuwa walimu hao sasa wanaweza kusoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi bila vikwazo.

Kwa mujibu wake, TSC pia imeendelea kuzipatia ofisi za wilaya vitendea kazi muhimu, ikiwemo pikipiki, kompyuta na mashine za uchapishaji (printer), hatua iliyoongeza ufanisi katika utoaji

wa umma, pamoja na kushughulikia mashauri ya kinidhamu kwa wakati.

Bw. Bahebe alisema matumizi ya Mfumo wa TSCMIS yameleta mageuzi makubwa katika utoaji wa huduma kwa walimu kwa kuwezesha usimamizi wa taarifa za walimu kidijitali, usajili wa waajiriwa wapya, usimamizi wa mikataba ya ajira na mashauri ya kinidhamu kwa ufanisi zaidi.

Alisema pia muundo mpya wa watumishi wa TSC umeboresha maslahi ya watumishi, kuongeza motisha wa kufanya kazi na kuimarisha utoaji wa huduma kwa walimu.

Aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuiwezesha TSC na kuweka mazingira bora ya utoaji wa huduma kwa walimu na watumishi wa Tume.

Akihitimisha, Bw. Bahebe aliishukuru Menejimenti ya TSC pamoja na Katibu wa Tume, Mwl. Paulina M. Nkwama, kwa kuendelea kuziimarisha ofisi za TSC ngazi ya wilaya kwa kuzitengea rasilimali na vitendea kazi vinavyoweza utoaji wa huduma bora kwa walimu na utekelezaji wa majukumu ya Tume.



Walimu wa ajira mpya Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani, wakifuatilia mafunzo elekezi yaliyoandaliwa na Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

TSC HANDENI YAIMARISHA ELIMU KINGA KWA WALIMU

Na Mwandishi Wetu – Handeni

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni imeendelea kuwekeza katika utoaji wa elimu kwa walimu kuhusu Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma kwa lengo la kuwajengea uelewa unaowasaidia kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kujiepusha na makosa ya kinidhamu.

Hayo yameelezwa hivi karibuni na Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Bi. Elizabeth J. Chikira, alipokuwa akizungumzia mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha huduma kwa walimu.

Bi. Chikira alisema Tume imekuwa ikitumia mbinu mbalimbali kufikisha elimu hiyo kwa walimu, zikiwemo mikutano, mafunzo elekezi kwa walimu wapya wanaojiriwa, semina, vipeperushi pamoja na miongozo mbalimbali inayowawezesha walimu kutambua haki na wajibu wao kwa wanafunzi, Serikali na jamii.

Aliiongeza kuwa Tume pia hutembelea shule ili kufahamu changamoto zinazowakabili walimu, hutoa mafunzo kwa kuwakutanisha walimu katika ngazi ya kata na kushiriki kutoa mada katika mikutano mbalimbali wanapoalikwa.

"Miongozo na elimu tunayoitoa

imewasaidia walimu kufahamu wajibu wao pamoja na masuala ya kinidhamu, ikiwemo kutambua makosa na hatua zinazoweza kuchukuliwa endapo watakiuka Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma," alisema.

Alisema Mwongozo wa Mafunzo Elekezi kwa Walimu Wapya umechangia kuwajengea uwezo walimu kuhusu sheria na kanuni zinazosimamia utumishi wao, jambo linalowasaidia kujiepusha na vitendo vinavyoweza kusababisha mashauri ya kinidhamu.

"Ualimu ni taaluma nyeti katika maendeleo ya Taifa. Ili kujenga kizazi chenye maadili na maarifa, ni lazima kuwa na walimu wanaotekeleza majukumu yao kwa weledi, uadilifu na uwajibikaji," alisisitiza.

Aidha, Bi. Chikira aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kuboresha sekta ya elimu kupitia ujenzi wa miundombinu ya elimu, utekelezaji wa sera ya elimu bila ada na maboresho ya mitaala yenye lengo la kuongeza ujuzi, umahiri na fursa sawa za kujifunza kwa wanafunzi nchini.

Alisema maboresho hayo yameongeza ari ya walimu katika utekelezaji wa majukumu yao na kuchangia kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

Katika hatua nyingine, alisema walimu 3,757 wa Wilaya ya Handeni walipandishwa vyeo kati ya mwaka 2021 na 2025, ambapo walimu wa shule za msingi walikuwa 1,805 na wa shule za sekondari 1,952.

Wakati huo huo, baadhi ya walimu wa Wilaya ya Handeni wameipongeza Serikali kwa kuendelea kuboresha mazingira ya kazi na utoaji wa elimu nchini.

Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kileleni, iliyopo Halmashauri ya Mji Handeni, Mwl. Horeza Mnyone Samweli, alisema Serikali imefanya maboresho makubwa katika sekta ya elimu na kushauri iendelee kuboresha maslahi ya walimu, kuimarisha maabara, kujenga nyumba za walimu na kuongeza mafunzo ya maendeleo ya kitaaluma.

Aidha, aliipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kuendelea kusimamia maslahi ya walimu, hususan katika maeneo ya upandishwaji wa vyeo, maadili na nidhamu, hatua ambazo zimeendelea kuinua hadhi ya



Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kileleni, Halmashauri ya Mji Handeni, Mwl. Horeza Mnyone Samweli, akitekeleza majukumu yake ya kufundisha.

taaluma ya ualimu.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule ya Msingi Kwamngumi, Mwl. Philomena Kilian Haule, alisema Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu kupitia ujenzi wa miundombinu na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

Aliishauri Tume kuendelea kutoa elimu kwa walimu kuhusu haki na wajibu wao pamoja na kushughulikia changamoto za kiutumishi, hususan upandishwaji wa vyeo, ili kuongeza ufanisi wa walimu na kupunguza makosa ya kinidhamu.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Kwamngumi, Halmashauri ya Mji Handeni, Mwl. Philomena Kilian Haule, akitekeleza majukumu yake ya kufundisha.



Kaimu Katibu Msaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Bi. Elizabeth J. Chikira, akitekeleza majukumu yake ofisini.

TSC HANDENI YAIMARISHA ELIMU KINGA KWA WALIMU

Afisa Maadili na Nidhamu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni, Bi. Agnes E. Kilonzo, akitekeleza majukumu yake ofisini.



Afisa wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Wilaya ya Handeni anayeshughulikia Ajira na Maendeleo ya Walimu, Bw. Fadhili R. Mdee, akitekeleza majukumu yake ofisini.



MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 **Barua Pepe:** secretary@tsc.go.tz **Tovuti:** www.tsc.go.tz



www.tsc.go.tz



Tume ya Utumishi wa Walimu